# UQAB
Jarida la



*Toleo 15 - Rajab 1439 AH / Aprili 2018 Miladi*

**TILLERSON: Huna La Kutatua**

**Ziara ya Balozi Mkuu wa Zamani wa Amerika Tillerson Barani Afrika ililenga Umwagaji Damu Zaidi ya Waislamu**

**Kampeni ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Elimu**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 11**

**SWALI/JAWABU: Ni Kipi Kilicho Nyuma ya Oparesheni ya Uturuki "Olive Branch" Kaskazini Mwa Syria?**

## Urusi Adui wa Uislamu na Waislamu




**Muokoe Mateka Jannat Bespalova!**

**Muko na Allah, Enyi Watu wa Al-Ghouta**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 14/1439 H | Ijumaa, 21 Jumadal Thani 1439 H | 09/03/2018 M

# Muko na Allah, Enyi Watu wa Al-Ghouta

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Zaidi ya mashambulizi ya angani 2000 yalifanywa na jeshi la anga la Urusi (mashambulizi 1150) na jeshi la anga la Syria (mashambulizi 900) na kuangamiza watu na ardhi; yaliangamiza mahospitali, masoko ya mboga na viwanda vya kuoka mikate, yakiuwa mashahidi 900 na kujeruhi raia 2000 wasiokuwa na silaha. Ulimwengu mzima umenyamazia kimya uchinjaji huu wa jambazi wa Damascus na Moscow, katika ukatili wao wa kuendelea kuwamaliza watu watu wa Ghouta, mashujaa waliokataa kumsujudia Firauni, au Nero wa karne hii, Bashar. Lakini Bashar si chochote isipokuwa ni kikaragosi aliyeyeapa majeshi ya anga ya Urusi "uhalali" katika uvamizi wao, unaomulika chuki nzito ya Putin kwa Uislamu na Waislamu.

Kimya cha nchi za Kimagharibi, zinazoitwa "jamii ya kimataifa", kinadhihirisha kushiriki kwao katika ukatili huu muovu. Nchi hizi tayari zilikwisha nyanyua mwito wa, "Katu Haitokei Tena" kuzuia kutokea upya kwa yale yanayoitwa mauaji ya halaiki (ya Ujerumani kwa Mayahudi). Huku mwito huu ukikosa kutabikishwa eneo la Srebrenica-Bosnia mnamo 1995, wakati ambapo majeshi ya kuhifadhi amani ya UM yalipo wasalimisha Waislamu kwa magengi ya wahalifu na kuwapa ruhusa ya kutekeleza mauaji ya halaiki dhidi ya Waislamu 11,000; wala haukutekelezwa nchini Rwanda mnamo 1994 wala nchini Afrika ya Kati mnamo 2016. Wala Myanmar mnamo 2017.

Ndio maana si ajabu kwa Kanali John Thomas wa afisi ya kushughulikia mambo ya umma katika taasisi kuu ya utoaji amri za kijeshi ya Amerika kuliambia gazeti la Daily Beast: "Hizo si kadhia zetu", "Taasisi kuu ya utoaji amri za kijeshi ya Amerika (CENTCOM) haihusiki na chochote nchini Syria isipokuwa tu kulishinda kundi la wanamgambo la ISIS na baadhi ya mamlaka ya kukabiliana na ugaidi",

Kumzuia gaidi mkubwa kabisa, Bashar Al-Assad, kibaraka mtiifu kwa Amerika, si sehemu ya mipango ya kijeshi ya Amerika nchini Syria. UM chini ya katibu mkuu katika masuala ya kisiasa Jeffrey Feltman,kwa kuendeleza mchezo wa jambazi huyu, alikiambia kikao cha Baraza la Usalama la UM mnamo 28/2/2018, juu ya hali ya kibinadamu nchini Syria, kwamba Umoja wa Mataifa utaendelea "kulingania haki na uwajibikaji kwa nguvu", "wale wanaohusika na msururu wa ugaidi unao athiri maisha ya kila siku nchini Syria… watahisabiwa",

Ruhusa hii inafafanua taarifa ya Lavrov: "Kuna makundi eneo la Mashariki mwa Ghouta pamoja na Idlib, ambayo yanawasilishwa kama makundi poa na washirika na wafadhili wa Kimagharibi, likiwemo kundi la Ahrar Al-sham na Jaish Al-Islam, yanayo shirikiana na vuguvugu la Ahrar Al-Sham", akiongeza kuwa serikali ya Syria na Moscow zitaendelea kuyalenga. Ndio. Lavrov analituhumu vuguvugu la Ahrar Al-Sham, linalopigana vita vikali dhidi ya Hay'at Tahrir Al-Sham mjini Idlib kwamba linashirikiana na kundi hili lilobandikwa jina la kuwa kundi la "kigaidi", ili kuhalalisha kampeni yao ya maangamivu kwa msingi wa sera ya uchomaji ardhi eneo la Ghouta.

Hiyo ndio sababu Urusi wala Umoja wa Mataifa hazikukubali ofa za kundi la Jaish Al-Islam na Failaq Ar-Rahman; kuondoa chembechembe za Hay'at Tahrir Al-Sham kutoka Ghouta. Kuziondoa chembechembe hizi kutaharibu kisingizio cha kupigana na magaidi. Na kuzibakisha ndani kutahalalisha ulipuaji mabomu kwa watoto na wanawake na kulipua mahospitali, masoko ya mboga, viwanda vya kuoka mikate, maduka ya madawa na magari ya dharura ya wagonjwa. Yote haya yako mbele ya macho na masikio ya "jamii ya kimataifa" ambayo inanyanyua bendera ya hadhara na haki za kibinadamu!

Na pia yako mbele ya macho na masikio ya watawala wa Waislamu walioshughulishwa na kuhudumia maslahi ya mabwana zao, wakoloni wa Kimagharibi. Na yako mbele ya macho na masikio ya viongozi wa majeshi katika biladi za Waislamu. Majeshi haya, yanayo nyonya maelfu ya mabilioni ya mali ya Waislamu, ikiwa hawata tekeleza majukumu yao ya kuwalinda Waislamu na kuhifadhi heshima na damu zao, ni lipi lengo la kuwepo kwao?

Mtume (saw) alisema: «مَا مِنْ امْرِئٍ يَخْذُلُ امْرَأً مُسْلِمًا فِي مَوْضِعٍ تُنْتَهَكُ فِيهِ حُرْمَتُهُ وَيُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ إِلَّا خَذَلَهُ اللَّهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ فِيهِ نُصْرَتَهُ وَمَا مِنْ امْرِئٍ يَنْصُرُ مُسْلِمًا فِي مَوْضِعٍ يُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ وَيُنْتَهَكُ فِيهِ مِنْ حُرْمَتِهِ إِلَّا نَصَرَهُ اللَّهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ نُصْرَتَهُ» "Hakuna mtu yeyote atakaye muacha mkono Muislamu yeyote katika hali ambayo utukufu wake unaangamizwa na heshima yake kudunishwa ndani yake, isipokuwa Allah naye atamuacha mkono katika hali ambayo inahitajia nusra ya Allah ndani yake, na hakuna mtu yeyote atakaye mnusuru Muislamu yeyote katika hali ambayo utukufu wake unaangamizwa na heshima yake kudunishwa ndani yake, isipokuwa Allah naye atamnusuru katika hali ambayo inahitajia nusra ya Allah".

Ewe Allah sisi ni wanyonge, tupe ushindi.

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ
يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

KUMB: 06/1439 H | Ijumapili, 23 Jumadal Thani 1439 H | 11/03/2018 M

# TILLERSON: Huna La Kutatua Kwani Mfumo Wako Muovu Wa Kibepari Unaangamiza Taifa Lako Na Ulimwengu Kwa Ujumla

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Waziri wa mambo ya nje wa Marekani Rex Tillerson yupo katika ziara ya mataifa matano ya Afrika ilioanza nchini Ethiopia siku ya Jumatano tarehe 7/03/2018.Kwa sasa yuko nchini Kenya na anatarajiwa kuzuru mataifa ya Chad, Nigeria na Djibouti. Ziara hii inatajwa kuangazia zaidi njia za kupambana na ugaidi na kustawisha usalama, biashara na suala zima uekezaji.

**Tunapenda kusema yafuatayo:**

Ziara ya Tillerson na waliomtangulia kabla yake inakuja ambapo taifa lake ni lenye kushuhudia mporomoko mkubwa wa kiuchumi uliosababishwa na tamaa yake ya kibepari ya kuvamia mataifa mengine na kumwaga damu za watu. Hali hii imefanya utawala wa Trump kukiri Marekani inaanguka hivyo ni lazima kuchukuliwe hatua za haraka na kupeana kipau mbele maslahi yake ya kiuchumi 'America First') dhidi ya washindani wake. Haya ni kama ilivyokuja ripoti iitwayo National Security Strategy iliochapishwa tarehe mwezi Disemba mwaka jana.

Mazungumzo kuhusu biashara na uekezaji tunayaona kama hatua ya Kiamerika kutaka kujikwamua kwake kiuchumi kupitia kupora rasilimali za mataifa ya Afrika chini ya madai ya kutaka kuiendeleza. Mataifa yenye nguvu hasa Marekani,Ulaya na China hudai kuipa Afrika mikopo na misaada wanayoitumia kama mbinu moja wapo ya kuendeleza ubeberu wao kiuchumi dhidi ya Afrika hali iliopelekea serikali nyingi za Kiafrika kujipata na limbikizi la madeni makubwa. Kwa sasa Kenya inatumia nusu ya mapato yake kulipia deni ambalo kwa ujumla sasa limefikia trilioni Ksh 5.4! Kwa masikitiko makubwa viongozi wa mataifa wamebakia kuwa mawakala na walinzi wa kulinda maslahi ya mabeberu wa kirasilimali matokeo yake kuifanya Afrika kuonekankwa kuwa bara masikini zaidi duniani!

Kuhusu suala la usalama na njia za kupambana ugaidi; twasema kuwa Marekani na washirika wake hawana nia ya kupambana na ugaidi kwani wao ndio wadhamini wa kuu wa ugaidi kote duniani. Majeshi ya Kimagharibi yanaongoza mashambulizi ya angani na ardhini kuwauwa watu wa Alepo na Alghouta ndani ya Syria.. Fauka ya haya, chini ya madai ya ugaidi Amerika imetia majeshi ya serikali nyingi hapa Afrika makwapani mwake na kuweka kambi zake za kijeshi kama mbinu yake ya kuyatoa mataifa ya Ulaya hasa Uingereza ndani ya Afrika ili yeye apate nafasi kubwa ya kupora Afrika. Na kwa haya mara nyingi harakati za mauaji hapa Afrika hudhaminiwa na Marekani ambaye huziita harakati za kuleta mageuzi.

Mwisho tunasema Juhudi zote hizi ni jaribio la Amerika kutaka kuziba aibu za mfumo wake na si kweli kuwa Marekani, Ulaya na Uchina yanatakia Afrika mema bali yote yana ajenda ya kuididimiza kwenye dhiki zaidi. Afrika. Hivyo twakariri kuwa Uislamu pekee ndio una uwezo wa kutatua matatizo ya bara kwa kupitia dola ya Khilafah ambayo sera yake ya kigeni haisimami juu ya ukoloni na ubeberu bali imesimama juu kueneza uadilifu kwa wanadamu wote.

**Shabani Mwalimu**
**Media Representative of Hizb ut Tahrir in Kenya**

# Ziara ya Balozi Mkuu wa Zamani wa Amerika Tillerson Barani Afrika ililenga Umwagaji Damu Zaidi ya Waislamu Kwa Kisingizio cha Mipango ya Vita Dhidi ya Ugaidi




**Habari:**

Ziara hiyo kama ilivyodokezwa na afisa mkuu wa Wizara ya Kigeni kama ufuatiliziaji juu ya mkutano kati ya Waziri Tillerson na mawaziri wa kigeni wa bara la Afrika jijini Washington mnamo Novemba 2017 ulioandaliwa kwa haraka na ambao uhudhuriaji wake ulikuwa mbaya. Ingawa mkutano huu wa mawaziri uligusia kadhia za kibiashara, maendeleo na usalama. Ziara ya mwisho ya Tillerson iliweka kipao mbele ushirikiano wa kiusalama na usaidizi wa Amerika kwa washirika wake muhimu barani Afrika katika vita dhidi ya al Shabaab nchini Somalia na Boko Haram Kaskazini Mashariki mwa Nigeria na eneo la ziwa Chad.

**Maoni:**

Sera ya Donald Trump ya kuiweka 'Amerika Mwanzo' inalenga kuwatazama wachezaji wengine ima kama washirika au mahasimu au vikwazo katika matarajio ya Amerika ya kisiasa ya kiulimwengu yeye akiwa kama bwana mkuu. Amerika kwa mtizamo wa sera hiyo ni lazima ilazimishe mamlaka yake na ijitanue kama mdhamini wa kiusalama wa kiulimwengu. Kufikia kiwango cha kukarabati na kuboresha sera yake nambari moja ambayo ni kuhakikisha kuwa Uislamu kama mfumo badili hausimami tena dhidi ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali ambao Amerika na washirika wake wanang'ang'ana katika

*Endelea Uk..5*

kuudumisha kutokana na kudhihirika kuporomoka kwake. Amerika iliamua kuzuru vibaraka wake wa Kiafrika wanaodaiwa kuwa washirika wakuu katika vita dhidi ya ugaidi na mapendekezo kwa kila mshirika kama yafuatayo:

**Kwanza,** Ethiopia, iliyo na jeshi kubwa na imara eneo hili, imekuwa ikipigana na al Shabaab tangu 2008. Nchi hiyo inakumbwa na mtafaruku mbaya wa kisiasa na kutojulika hatima yake, lakini ziara ya Tillerson jijini Addis ilitawaliwa na wasiwasi wa kiusalama. Alitumia ziara yake kuhakikisha upya usaidizi wa Amerika kwa serikali hiyo, na kutahadharisha serikali hiyo kutoruhusu kadhia za kindani za kisiasa kuipoteza mwelekeo kutokana na juhudi za vita dhidi ya ugaidi eneo hilo.

**Pili,** Djibouti, nchi ndogo sana yenye idadi ya wakaazi chini ya milioni moja, imehudumu kama kitovu cha oparesheni za Kiamerika eneo hilo. Huku kimikakati ikiwa iko kaskazini mwa Somalia na upande wa pili wa Bahari Nyekundu kutoka nchi iliyo sambaratishwa na vita ya Yemen. Djibouti ni makaazi ya maelfu ya majeshi ya Amerika katika kambi ya Lemonnier, ambayo ni idadi kubwa zaidi ya mkusanyiko wa majeshi ya Amerika barani Afrika. Maadamu al Shabaab bado ni tishio nchini Somalia, kambi ya Lemonnier itakuwa ndio kitovu cha mtandao wa mashambulizi ya Amerika eneo hilo. Ziara ya Tillerson nchini Djibouti pia ililenga kukabiliana na kukua kwa ushawishi wa China na uwepo wake nchini humo. Katika muongo uliopita, China imemimina mamilioni ya dolari ndani ya kijinchi hicho kidogo na imekuwa ikifanya bidii kujimakinisha kuwa mshirika nambari moja wa maendeleo na usalama wa Djibouti. Hivi majuzi Beijing ilikamilisha miradi miwili mikuu nchini Djibouti: mradi wa mamilioni ya dolari wa barabara ya reli kuelekea nchini Ethiopia na kambi ya kwanza ya kijeshi ya China ng'ambo, jengo pana linaloshinda lile la Amerika.

**Tatu,** Kenya, ambayo imekuwa mlengwa wa mashambulizi mabaya ya kigaidi kutoka kwa al Shabaab, iko na maelfu ya vikosi vyake nchini Somalia kama sehemu ya AMISOM. Hivi majuzi ujumbe wa Muungano wa Afrika nchini Somalia, Amisom, ambao majeshi ya Kenya, KDF, ni sehemu yake, uliungama juu ya muda wake wa kujiondoa kutoka Somalia kufikia 2020 na kusema kuwa muda huo hauna hakika. Tillerson alikwenda kuihakikishia upya Kenya, mshirika wa kale wa kiusalama wa Amerika eneo hilo, kuendelea kwa Washington kutoa usaidizi wa kijeshi, kijasusi na kifedha ili kubakia vitani nchini Somalia.

**Nne,** Nigeria, mahusiano ya kiusalama kati ya Amerika na Nigeria daima hayaja kuwa shwari na maafisa wa Nigeria siku za nyuma wamekiuka mipaka ya Amerika katika ununuzi na umiliki wa zana za kijeshi za Kiamerika, hususan rasilimali za ndege. Tillerson alikwenda kuwahakikisha upya usaidizi wa Amerika kwa Nigeria huku akishajiisha maafisa wake kuzidisha vita dhidi ya Boko Haram na kuimarisha ushirikiano wao na dola nyenginezo eneo hilo ambako Boko Haram inaendesha shughuli zake.

**Tano,** Chad, mwanachama imara zaidi wa G-5, mtandao wa mataifa matano ya kieneo yanayo pigana vita dhidi ya ugaidi dhidi ya Boko Haram eneo hilo, Chad imefedheheshwa na kutajwa na utawala wa Trump kama moja ya nchi nane kuu za Waislamu ambazo raia wake wamepigwa marufuku ya kusafiri nchini Amerika. Tillerson alikwenda kuwashukuru maafisa wa Chad kwa dori yao wanayo cheza katika kupigana na Boko Haram huku akiwahakikishia upya kimya kimya kwamba Wizara ya Kigeni ya Amerika itafanya kila iwezalo kuitoa Chad kutoka kwa orodha ya nchi zilizo athirika na marufuku hiyo ya usafiri.

Kwa kutamatisha, licha ya majaribio kadhaa ya uongozi wa Amerika ambayo mikononi mwake damu inachirizika na washirika wake kuukoa mfumo wao batili wa kisekula wa kirasilimali kutokana na kuporomoka, Umma wa Kiislamu utabakia imara na kupinga walinganizi wote wa batili walio dhidi ya mwamko na kushikamana juu ya mradi wa Khilafah ambayo itasimama tena hivi punde kwa njia ya Mtume (saw) kwa baraka na usaidizi wa Allah (swt).

إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ

**Kwa hakika, makafiri hawafanikiwi.**
[Al-Muminoon: 117]

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Kampeni ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir "Muokoe Mateka Jannat Bespalova!"

Kutokana na maafa yanayo tekelezwa na serikali ya kihalifu ya Urusi dhidi ya Waislamu wa Urusi, leo, mamia ya Waislamu wanafungwa katika magereza ya Urusi kwa sababu ya kushiriki kwao katika kazi ya Hizb ut Tahrir. Walituhumiwa "ugaidi" kirongo kwa kutegemea uamuzi wa kufedhehesha wa Mahakama ya Upeo wa kuiorodhesha Hizb ut Tahrir kama shirika la kigaidi. Kwa mujibu wa uamuzi huu wa kiajabu, Chama hiki cha Kisiasa cha Kiislamu, kikawa chama cha "kigaidi".

Kutokana na mkazo wa sheria za Urusi dhidi ya wanachama wa chama hiki, mashtaka yakazuliwa sio kwa msingi wa sheria za "siasa kali" katika katiba bali kwa msingi wa sheria za "ugaidi"; ambapo vifungo vinaweza kufikia mpaka miaka ishirini gerezani.

Utekelezaji "sheria" hizi ulipelekea kufungua mwanya wa mateso katika maeneo yote ya Urusi, ikiwemo St. Petersburg, ambako idadi kubwa ya wabebaji ulinganizi wamekamatwa katika muda wa miaka michache iliyopita. Mnamo tarehe 24 Novemba huduma za usalama zilimkamata mke wa mmoja wa wafungwa aliye hukumiwa miaka 12 gerezani, naye ni, Issa Rahimov mwanachama wa Hizb ut Tahrir. Mkewe Issa ni mwenye asili ya Kirusi; alisilimu na kubadilisha jina lake kutoka Allan na kuwa Jannat Bespalova. Alikamatwa kwa kufanya kazi kwake na Hizb ut Tahrir na kutupwa gerezani ambamo wahalifu huzuiliwa. Hatimaye iliamuliwa, mnamo Januari 2018, kuongezwa muda wa kifungo cha dada huyu kwa miezi miwili mengine, hii ikimaanisha atasalia ndani ya magereza ya Urusi hadi 16/03/2018, tarehe inayofuata ya kusikizwa kesi kotini. Allah (swt) asema:

قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الآيَاتِ إِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ

"Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini" [Al-i-Imran: 118]

Kutokana na matukio yote haya, Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir imeanzisha kampeni ya kiulimwengu inayoitwa "Muokoe Mateka Jannat Bespalova!" Jibu muwafaka kwa matendo ya Urusi dhidi ya wanawake wanyonge wa Kiislamu, ni kufanya kazi na Hizb ut Tahrir kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Hii ndio njia sahihi ya kupata radhi za Allah (swt). Kuregesha utawala wa Kiislamu kutawapa afueni Waislamu kutokana na sheria za kikafiri na uovu wa serikali za kidhalimu. Allah (swt) asema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo lenye kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." [Al-Anfal: 24].

Ewe Allah, tunakuomba usaidizi wako na umbariki dada yetu Jannat kwa himaya yako, na mumewe na Waislamu wote wanaozuiliwa katika magereza ya makatili pasi na kosa lolote; na Waislamu wanaodhalilishwa kwa sababu ya kubeba kwao ulinganizi wa Kiislamu. Ewe Allah, tunakuomba uilete karibu siku ile ambayo Waislamu wataregesha tena utawala wa Uislamu ardhini, kwa nusra yako, na kuwaadhibu wale wote waliowashambulia vijana na mabinti wa Umma wetu mtukufu, Ewe Allah ikubali dua yetu, Ameen.

**Hashtag za Kampeni:**
**#SaveJanat**
**أنقذوا_جنات#**
**#ДжаннатБеспалова**
**Jumamosi 15 Jumada Al-Akhir 1439 H - 03 Machi 2018 M**



### Elimu ni nini?

Elimu ni mpangilio wa kuwezesha kusoma, au kupata ujuzi, maadili, itikadi, na tabia. Mbinu za kielimu zinajumuisha utoaji hadithi, majadiliano, usomeshaji, ufunzaji, na muongozo wa utafiti. Elimu mara nyingi hupatikana chini ya muongozo wa walimu, lakini wanafunzi waweza pia kujielimisha peke yao. Elimu huweza kupatikana katika mazingira rasmi au yasiyo rasmi na hali yoyote itakayo leta athari ya namna mtu anavyo fikiri, anavyo hisi, au anavyo tenda huenda ikakadiriwa kama hali ya kielimu.

### Malengo Yenye Kujengea Hoja Elimu

Thaqafa ya taifa lolote ndio uti wa mgongo wa kuwepo na kudumu kwake. Kwa msingi wa thaqafa hii, hadhara ya Umma hujengwa juu yake, na malengo na dhamira yake hufafanuliwa, na mfumo wake wa kimaisha kubainishwa. Watu wa Umma huo huundwa na kuyayushwa kwa thaqafa hii ndani ya chungu kimoja kiasi ya kuwa Umma huo unakuwa Umma wa kipekee tofauti na mataifa mengine. Thaqafa hii ndio itikadi ya kifikra ya Umma huo na sheria, masuluhisho na nidhamu zake huchipuza kutokamana na itikadi hii ya kifikra. Pia elimu na sayansi hujengwa juu yake, pamoja na matukio yanayo nasibishwa na itikadi hii ya kifikra kama vile Seerah ya Umma na historia yake. ikiwa thaqafa hii itatoweka, Umma huu, kama Umma wa kipekee, utapotea; hivyo basi lengo lake na mfumo wake wa kimaisha yatabadilika, na utiifu wake utagura, na utaporomoka katika njia yake kwa kufuata thaqafa za mataifa mengine.

### Elimu Nchini Kenya:

### A: Kabla ya Enzi ya Ukoloni

Wakati huo elimu ulikuweko katika mazingira yasiyo rasmi kisha baadaye kugeuka na kuwa katika

*Endelea Uk..8*

mazingira rasmi kuanzia mwaka wa 1728 wakati wa kuwasili kwa wafanyi biashara waarabu waliowafunza watu katika maeneo waliofanyia biashara jinsi ya kusoma, kuandika na hata kuzungumza lugha ya kiarabu, ambayo ilikuwa ni muhimu katika kusoma na kuelewa Quran, na kupelekea kusilimu na kueneza Uislamu. Kisha, wamisheni wa kikristo wa kimagharibi kupitia jumuia ya kimisheni ya kanisa (CMS) waliwasili nchini Kenya mnamo 1846 na kuasisi shule ya kimisheni eneo la Rabai jijini Mombasa na kuanza kufunza ukristo na ujuzi msingi ambapo baadaye waliohitimu waliingia katika ukristo na wakatumiwa kusukuma mbele kazi ya umisheni eneo hilo na kuhudumu kama watumishi wa kikoloni katika utawala wa kikoloni unaokuja.

**B: Ukoloni**

**Taarifa ya Sera ya Elimu**

Elimu ilikuwa ni haki msingi kwa walowezi wa kizungu katika kupata ujuzi wa kazi za kiofisi ulio muhimu katika kutekeleza majukumu ya kiidara ya kikoloni. Lakini, elimu kwa Waafrika ilikuwa ni fadhila tu kwao ili kuzalisha nguvu kazi iliyo elimika kiasi tu itakayo tumiwa kama vibaraka na machifu katika idara ya kikoloni. Natija yake, ni kuimarisha uchumi wa kikoloni kwa kufunza ujuzi katika ukulima, useremala, uashi na kazi nyenginezo za kiufundi kwa wengi wa Waafrika ili wafanye kazi kwa gharama nafuu kwa jamii ya walowezi wa kizungu. (Sera hii ya elimu iliwafanya Waafrika kupinga na kusababisha kufungua shule huru zao wenyewe ambapo mara nyingi ilipelekea mgongano baina yao na serikali ya kikoloni).

**Taswira Fupi ya Hali ya Elimu ya Kikoloni Nchini Kenya**

Mnamo 1929, kanisa la Scotland, jumuia ya injili ya kimisheni na misheni ya nyanda za juu ya Afrika (AIM) ziliwaagiza wafuasi na walimu wake kupinga tohara ya wanawake. Wale ambao hawakutii agizo hili walipoteza ajira na kufukuzwa makanisani. Hatimaye mnamo 1930, utawala wa kikoloni ulilazimika kuja na waraka wa sera nyengine iliyo julikana kama waraka mweusi wa mwaka 1930. Waraka huo ulikariri kuwa elimu ya Waafrika ni sharti ilenge kuwafanya Waafrika kushiriki katika mambo ya maeneo yao wanayoishi. Mapendekezo ya waraka huo mweusi wa mwaka 1930 pamoja na upinzani wa wamisheni dhidi ya tohara ya wanawake yalipekea kuasisiwa kwa shule huru nchini Kenya baada ya 1930. Chuo cha Walimu wa Kiafrika cha Kenya (K.A.T.C) kiliasisiwa eneo la Githunguri mnamo 7 Januari, 1939. Chuo hicho kililenga kuzalisha walimu kwa ajili ya shule hizo huru. Kupanuka kwa shule huru kulitokana na kuzuka kwa vita vya pili vya dunia mnamo 1939-1945. Walimu wapiganaji wa kizungu walirudi kwao kusaidia kuhami nchini yao na walimu wa kiafrika walivutiwa na jeshi hilo kwa sababu lilitoa mishahara mizuri kuliko ualimu. Hii ilipelekea upungufu wa walimu katika shule za kisekula za kimisheni. Upungufu huu ulikuwa na natija nzuri kwa shule huru. Ulipelekea Waafrika kuimarisha elimu yao huru. Haja ya kutaka elimu zaidi na bora iliwaingia wapiganaji Wakongwe. Walikuwa wamesafiri nje ya Kenya na kushauriana na wenzao kutoka katika koloni kama ya India juu ya aina ya elimu inayotolewa na serikali ya kikoloni. Aina hii ya elimu ilisaidia pakubwa katika mvutano wa ukombozi dhidi ya ugandamizi wa kizungu.

Mnamo 1951, shule nyingi huru zilipinga mapendekezo ya Tume ya Beecher iliyo buniwa mnamo 1949 iliyo pendekeza kuelimishwa tu kwa Waafrika wachache huku wengi wao wakisalia kama vibarua ndani ya mashamba ya wazungu. Natija yake, mnamo 1952, idara ya kikoloni ilitangaza hali ya hatari. Viongozi wa vuguvugu la shule huru walikamatwa na shule huru kufungwa baada ya kukataa kuwa chini ya usimamizi wa Bodi ya Elimu ya Wilaya au Misheni na kutuhumiwa kuhusika na kundi la waasi la Mau Mau.

**C: Enzi Baada ya Ukoloni**

***A: Taarifa ya Sera ya Elimu***

Elimu ni haki msingi ambayo ni lazima ipeanwe kwa kila Mkenya, kulingana na misingi ifuatayo: usawa wa kisiasa, umoja wa kitaifa, adilifu wa kijamii na hadhi ya kibinadamu, uhuru wa kidini na maadili, uhuru wa ujinga na maradhi, fursa sawa kwa raia wote bila ya kujali tabaka, dini, jinsia au rangi, ugavi sawa wa mapato ya kitaifa na kuimarisha na kuhifadhi turathi ya kitamaduni.

***B: Malengo Jumla ya Elimu***

Elimu nchini Kenya imejengwa juu ya sheria ya elimu kifungu cha 211 ya mwaka 1968 iliyo rekebishwa 1970 na 1980 kama stakabadhi kuu ya kisheria inayo simamia elimu. Sheria hii inaagiza kuanzishwa kwa shule, idara na usimamizi, kuimarishwa kwa elimu ya ziada na ya darasani. Malengo ya elimu nchini Kenya kama yalivyo fafanuliwa na iliyo kuwa Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE) ambayo sasa inajulikana kama Taasisi ya Uundaji Mtaala wa Elimu ya Kenya (KICD) ni:

1. Kuimarisha utaifa, uzalendo na umoja wa kitaifa.
2. Kuimarisha maendeleo mtu binafsi na kujitosheleza kibinafsi.
3. Kuimarisha heshima na maendeleo kwa utajiri wa tamaduni tofauti tofauti za Kenya.
4. Kuimarisha utambuzi wa kimataifa na kukuuza hisia nzuri kwa mataifa mengine.
5. Kuimarisha mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na ya kiviwanda kwa ajili ya maendeleo ya kitaifa.
6. Kuimarisha hisia nzuri kwa afya bora na hifadhi ya kimazingira.

***C: Hatua za Elimu***

Baada ya uhuru, Kenya pamoja na koloni nyengine za Kiingereza za Uganda na Tanzania ziliungana chini ya Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) kutabikisha mfumo wa elimu wa Kiingereza wa 7-4-2-4 kwa miaka kumi. Wanafunzi wa

***Endelea Uk..9***

shule za msingi walikalia mtihani wa Shahada ya Elimu Msingi ya Afrika Mashariki (EACPE). Huku wanafunzi wa shule za upili wakikalia mtihani wa Shahada ya Elimu ya Afrika Mashariki (EACE). Kisha kwa wale wanaopendelea kuendelea na kiwango cha chuo kikuu walilazimika kukalia mtihani wa Shahada ya Juu ya Elimu ya Afrika Mashariki (EAACE). Mnamo 1977, Jumuia ya EAC iliporomoka kutokana na Amerika kufaulu kuchukua udhibiti wa Uganda na Tanzania lakini Kenya ikabakia chini ya mkono wa Uingereza na hivyo, kuendelea na mfumo ule ule wa elimu lakini ikabadilisha majina ya mitihani kutoka kwa utambulisho wake wa kieneo kuwa utambulisho wa kitaifa. Shahada ya Elimu Msingi ya Afrika Mashariki ikawa Shahada ya Elimu Msingi (CPE), Shahada ya Elimu ya Afrika Mashariki ikawa Shahada ya Elimu ya Kenya (KCE) na Shahada ya Elimu ya Juu ya Afrika Mashariki ikawa Shahada ya Elimu ya Juu ya Kenya (KACE).

Mnamo 1985, Raisi Moi alianzisha mfumo wa 8-4-4. Kwa kuanzishwa mfumo huu wa 8-4-4 mtihani wa CPE ukawa KCPE huku mtihani wa KCE ukiwa KCSE. Uamuzi huu ulitokana na kuwa mfumo wa 7-4-2-4 ulikosa maalumati muhimu ya kuimarisha utoaji ajira ya kujitegemea badala yake uliangazia tu namna ya kuwatayarisha wasomi kwa kazi za kuajiriwa maofisini.

Mnamo 2018, Raisi Uhuru Kenyatta alianzisha mfumo wa 2-6-3-3-3 ambao utakuwa miaka 2 ya chekechea, miaka 6 ya msingi, miaka 3 ya msingi ya juu, miaka 3 ya upili ya chini na miaka 3 ya upili ya juu kwa miaka yote 17 wanafunzi hawatakalia mitihani badala yake watakuwa wakitahiniwa kupitia majaribio ya kuendelea (CAT) juu ya ujuzi waliopata kinyume na kuhifadhi maalumati kwa ajili ya mitihani kama ilivyo kuwa hali katika mfumo uliopita. Uamuzi huu ulitokana na mfumo wa elimu wa 8-4-4 kukosa maalumati muhimu ya kuimarisha ajira ya kibinafsi.

**Matokeo ya Utekelezaji Nidhamu ya Elimu ya Kirasilimali:**

1. Uzalishaji idadi kubwa ya ‘raia’ waliolemaa kisiasa, wenye kujisalimisha, mabwege, wasio jitolea pakubwa mbali na miaka 15 na zaidi ya ‘elimu’ yao, kutafiti kwa kina matatizo msingi ya jamii yao. Baada ya hapo, kusoma sana katika mazingira ya kiimla hivyo basi huachia utendakazi wa jamii yao kwa uongozi na ujuzi uliopo. Kamwe hawaoneshi hamu ya kuchukua udhibiti wa hatma yao jumla na wala hawaulizi achilia mbali kupinga dhulma za kisiasa na za kijamii na kiuchumi wanazofanyiwa juu yao.

2. Uzalishaji wafanyi kazi. Wamefunza ujuzi na cha muhimu zaidi, nafsiya inayo hitajika kwa wafanyi kazi mashini za viwanda kwa utiifu, kujitolea na wafanyi kazi wenye ujuzi watakao kubali uongozi na mamlaka, kuchunga wakati, kuwa na bidii, kufanya wanacho ambiwa, kula na kutotarajia kuwa na udhibiti kwa hali yao.

3. Kuhalalisha msimamo wa kijamii na ubaguzi. Wale wanaofeli shuleni huona kuwa hawana ‘akili’ na hivyo hawastahili kazi na fursa nzuri za maisha. Hii inachangia kufanya ubaguzi ndani ya jamii kuwa usiokuwa na budi na halali.

4. Uzalishaji wa washindani, watu wanaoamini na kupenda ushindani hivyo, mshindi huchukua jamii nzima. Hujiona kama wanaostahili fursa walizozichuma kwa tabu. Huku washindwa wakionekana kama wanaostahili hatma yao. Huangazia namna ya kuendeleza maslahi yao binafsi bila ya kutilia maanani manufaa jumla ya watu hivyo, kuhalalisha nidhamu inayo pendelea matajiri wakubwa kujitanua.

5. Uzalishaji watumizi wenye ari. Watu, wanaojali tu kusonga mbele, kufanikiwa na kutajirika, pamoja na kutafuta maendeleo ya kisasa, kujitanua kwa nidhamu za kimagharibi kama lengo la maisha; na wanao kubali mfumo wa masoko na kudhani kuwa weledi wa kiteknolojia ndio utakao tatua matatizo yao. Kama walivyo lemazwa na utekelezaji vitendo vyao, kufanya kazi kwao, na maamuzi yaliyo wasilishwa kwao na walimu wao hivyo, pia wamelemaa katika utumizi wao wa bidhaa, huduma na maamuzi yaliyo wasilishwa kwao na serikali, mashirika na mabwenyenye wataalamu.

6. Viwango vya kushtua vya ukosefu wa ajira kutokana na masomo yanayo endekeza shahada, ambapo wengi wa wanafunzi wamejifunga tu na kuangazia namna ya kupata shahada hizi kama njia ya kuhalalisha uwezekano wa kuajiriwa kinyume na masomo yanayo elekeza katika ujuzi na thamani yake ambayo yamekosekana katika taasisi nyingi za masomo.

**Elimu Ndani ya Khilafah**

**A: Taarifa ya Sera ya Elimu**

Nidhamu ya elimu ndani ya dola ya Khilafah imeundwa kwa ukamilifu wa hukmu za kisheria na kanuni za kiidara zinazo husiana na mtaala wa elimu. Hukmu za kisheria zinazo husiana na elimu zimechipuza kutokana na itikadi ya Kiislamu na zina dalili zake za kisheria, kama vile masomo yanayo someshwa na kutenganishwa baina ya wanafunzi wa kiume na wa kike. Ama kuhusu kanuni za kiidara zinazo husiana na elimu, ni mbinu na miundo inayojuzu, ambayo mtawala aliye mamlakani huzikadiria zenye manufaa katika utabikishaji nidhamu hii na kufikia malengo yake. Ni miongoni mwa mambo ya kimadania yanayo hitajika kwa ajili ya maendeleo na hubadilika kulingana na yale yanayo onekana kuwa munasibu katika utabikishaji wa hukmu za kisheria zinazo husiana na elimu na mahitaji msingi ya Umma. Vile vile, yanaweza kutabanniwa kutokana na majaribio, ujuzi na utafiti unaojuzu kutoka kwa mataifa mengine.

**B: Malengo Jumla ya Elimu**

Kuna malengo mawili makuu ya elimu ambayo ni lazima yazingatiwe

*Endelea Uk..10*

wakati wa kuunda mbinu na masomo ya elimu:

1. Kuunda shakhsiya ya Kiislamu inayo jumuisha ufahamu (aqliyyah) na utendakazi (nafsiyyah), kwa watoto wa Umma kupitia kuzamisha thaqafa ya Kiislamu inayo jumuisha itikadi ya Kiislamu, fikra na miondoko – ndani ya aqliyya na nafsiya za wanafunzi. Kwa hayo, umakinifu ni lazima utekelezwe na wale waliopewa jukumu na dola ya Khilafah kuunda na kutabikisha mbinu kufikia lengo hili.

2. Kuwatayarisha watoto wa Kiislamu kiasi ya kuwa baadhi yao waje kuwa wanazuoni wenye ujuzi katika kila nyanja ya maisha ima katika sayansi za Kiislamu (Ijtihad, Fiqh, Ukadhi nk) au Sayansi za kiufundi (Uhandisi, Kemia, Fizikia, Udaktari nk). Wasomi walio na uwezo wa kuibeba dola ya Kiislamu na Umma juu ya mabega yao ili kupata nafasi ya uongozi miongoni mwa mataifa na dola za kiulimwengu, kiasi ya kuwa Khilafah iwe ndio Dola inayo ongoza na yenye ushawishi mkubwa juu ya mfumo wake, na wala sio Dola ndogo au Dola kibaraka katika fikra yake na uchumi wake.

**C: Hatua za Elimu**

Kwa msingi wa dalili na hukmu za kisheria, hatua za usomeshaji shule ndani ya Dola ya Khilafah zinagawanyika juu ya msingi wa umri wa mwanafunzi na wala sio masomo yanayo someshwa na shule. Shule zinagawanyika aina tatu katika mpangilio ufuatao: mfumo wa 4-4-4, ambayo ni miaka 4 ya kiwango cha msingi (baina ya umri wa miaka 6 – 10), miaka 4 ya kiwango cha shule ya wastani (baina ya umri wa miaka 10 – 14) na miaka 4 ya kiwango cha shule ya upili (baina ya umri wa miaka 14 – 18).

**C: Taswira Fupi ya Hali ya Elimu Ndani ya Khilafah Kabla ya Kuvunjwa Kwake**

Miaka elfu moja iliyo pita, vyuo vikuu maarufu vilikuwepo mjini Gundishapur, Baghdad, Kufah, Isfahan, Cordoba, Alexandria, Cairo, Damascus, na katika miji kadhaa mengine ya biladi za Kiislamu. Elimu ya juu nje ya Dola ya Khilafah wakati wa zama hizo ilikuwepo pekee kostantinia, Kaifeng (Uchina), na Nalanda (India). Na hata zama hizo, Chuo Kikuu cha kostantinia kilikuwa kikiiga vyuo vikuu vya Baghdad na Cordoba. Katika Ulaya Magharibi, zama hizi, hakukuwa na hata chuo kikuu kimoja. Chuo kikuu cha zamani zaidi nchini Italy ni chuo kikuu cha Bologna kiliasisiwa mnamo 1088. Chuo Kikuu cha Paris na Chuo Kikuu cha Oxford viliasisiwa baina ya karne ya 11 na 12, na hadi kufikia karne ya 16 vilikuwa vikiagiza vitabu kutoka kwa ulimwengu wa Kiislamu.

Kozi nyingi za elimu ya juu ndani ya Dola ya Kiislamu ya Khilafah zilichangia katika kuinua hadhara ya Kiislamu. Maelfu ya miaka kabla ya zama za ‘Wright Brothers’, Abbas ibn Firnas alifanya majaribio kadhaa ya kuunda mashini inayo paa. Katika mwaka wa 852, aliruka kutoka juu ya mnara wa msikiti wa Cordoba, akiwa amejitatia nguo iliyo kazanishwa na papi za mbao. Ibn Ismail ibn al Razzaz Al-Jazari, alikuwa mwanasayansi na mhandisi aliyefaulu kuunda robot wa kwanza duniani katika karne ya 12. Aliishi eneo la Mesopotamia na kufanya kazi kwa miaka 25 katika kasri la Sultan Nasir Al-din Mahmoud. Mbali na kufaulu kuunda teknolojia ya robot, pia aliunda vifaa vilivyo rahisisha kazi za mwanadamu, kwa kuziunda ili kutumika kiotamatiki kwa juhudi ndogo za mwanadamu. Mbali na hili, kulikuwa na tafiti na uvumbuzi mwingi zaidi katika zama za Khilafah zilizo badilisha sura ya ulimwengu.

**D. Matokeo ya Utekelezaji Nidhamu ya Elimu ya Kiislamu:**

1. Uzalishaji wasomi wa Kiislamu walio na kiwango cha juu cha shakhsiya ya Kiislamu waliobobea na tajriba katika nyanja zote za thaqafa ya Kiislamu.
2. Uzalishaji wa jopo kazi lenye uwezo wa kuhudumia maslahi msingi ya Umma, pamoja na jopo kazi lenye uwezo wa kupanga mikakati ya muda mfupi na muda mrefu.
3. Utayarishaji jopo kazi muhimu la kuchunga mambo ya Umma, kama uzalishaji madaktari, walimu, mauguzi, wahandisi wa kutosha na wengineo katika taaluma muhimu kwa ajili ya mahitaji ya watu na dola.

**Mukhtasari**

Elimu ni kifaa muhimu cha kulinda na kuhifadhi thaqafa ya taifa na hutegemea juu ya mambo kadhaa lakini la muhimu ya yote ni kadhia ya kisiasa inayotokana na itikadi msingi za dola zinazo amua mafanikio yake au kufeli kwake. Kwa uhalisia, nidhamu ya elimu iliyo chukuliwa kutoka kwa enzi za ukoloni pamoja na enzi baada ya ukoloni ililenga kuwahujumu na kuwanyanyasa watu kwa misingi ya kitabaka na rangi na kuwafanya watumwa kwa manufaa ya hali halisi ya wakati ule na leo. Kinyume na nidhamu ya elimu chini ya Khilafah itakayo simama tena hivi punde kwa njia ya Mtume (saw), itokayo kwa Muumba na kutabikishwa ili kuwasilisha shakhsiya ya Kiislamu ndani ya watu na kuwageuza watu kutumia elimu katika kutafuta radhi za Muumba wao bila kujali rangi, tabaka, kabila nk.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 11: Mivutano ya Kifikra Katika Da’wah ya Mtume (saw)



Katika halaqah hii tunaendelea na hatua ya tatu katika njia ya Mtume (saw) kuleta mageuzi. Leo tutazungumzia kuhusu mivutano ya kifikra ndani ya da’wah ya Mtume (saw)

**Mvutano wa kifikra katika Aqeeda**

Ili iwe hukmu ni ya Allah pekee, na kupwekeshwa katika ibada, Alikuwa Rasul (saw) akipambana na imani za kikafiri na za kishirikina za waliokuwa wakiabudu masanamu. Akawa anawasomea kauli ya Allah (swt):

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَآ إِبْرَٰهِيمَ رُشْدَهُۥ مِن قَبْلُ وَكُنَّا بِهِۦ عَٰلِمِينَ

Na hakika tulikwisha mpa Ibrahim uwongofu wake zamani na tulikuwa tunamjua.

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِۦ مَا هَٰذِهِ ٱلتَّمَاثِيلُ ٱلَّتِىٓ أَنتُمْ لَهَا عَٰكِفُونَ

Alipomwambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayo yashughulikia kuyaabudu?

قَالُوا۟ وَجَدْنَآ ءَابَآءَنَا لَهَا عَٰبِدِينَ

Wakasema: tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.

قَالَ لَقَدْ كُنتُمْ أَنتُمْ وَءَابَآؤُكُمْ فِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ

Akasema: Bila ya shaka nyinyi na baba zenu mmekuwa katika upotofu ulio dhaahiri.
[Al-Anbiya: 51-54]

Na (saw) akawasomea:

قالَ أَفَتَعبُدونَ مِن دونِ اللَّهِ ما لا يَنفَعُكُم شَيئًا وَلا يَضُرُّكُم

Akasema: Basi nyinyi mnawaabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu wasio kufaini kitu wala kukudhuruni?
[Al-Anbiya: 66]

Na (saw) akawasomea:

إِنَّكُم وَما تَعبُدونَ مِن دونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُم لَها وارِدونَ

Hakika nyinyi na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu; huko mtaingia tu.
[Al-Anbiya: 98]

*Endelea Uk..12*

**Mvutano wa Kifikra Katika Mila na Mazoea**

Ili kubainisha uadilifu wa nidhamu ya Kiislam, alikuwa Rasul (saw) alipambana na fikra za watu wajinga zinazofungamana na mila na mazoea ambazo zilikuwa zimetanda wakati huo, ikawa ni kwa njia ya kuzihujumu mila. Mfano ni kuzika watoto wa kike wakiwa hai; akawa (saw) anawasomea kauli ya Allah Ta'ala:

وَإِذَا المَوءودَةُ سُئِلَت

Na msichana aliye zikwa hai atapo ulizwa,

بِأَيِّ ذَنبٍ قُتِلَت

Kwa kosa gani aliuliwa?
[At-Takwir: 8-9]

Na (saw) akawasomea:

وَإِذا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالأُنثىٰ ظَلَّ وَجهُهُ مُسوَدًّا وَهُوَ كَظيمٌ* يَتَوارىٰ مِنَ القَومِ مِن سوءِ ما بُشِّرَ بِهِ ۚ أَيُمسِكُهُ عَلىٰ هونٍ أَم يَدُسُّهُ فِي التُّرابِ ۗ أَلا ساءَ ما يَحكُمونَ

Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyo bashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyo hukumu! [An-Nahl: 58-59]

**Mvutano wa Kifikra Katika Maisha**

Ili kubainisha ukubwa wa nidhamu ya kiuchumi ya kiislamu, alikuwa Rasul (saw) alipambana na nidhamu ya kiuchumi ya kijahilia iliokuwa ikiendelea zama hizo. Akawa anahujumu muamala wa riba, Na kazi ya kupunja vipimo; Na alikuwa (saw) akiwasomea:

وَما آتَيتُم مِن رِبًا لِيَربُوَ في أَموالِ النّاسِ فَلا يَربو عِندَ اللَّهِ ۖ وَما آتَيتُم مِن زَكاةٍ تُريدونَ وَجهَ اللَّهِ فَأُولٰئِكَ هُمُ المُضعِفونَ

Na mnacho kitoa kwa riba ili kiongezeke katika mali ya watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mnacho kitoa kwa Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio watao zidishiwa.
[Ar-Rum: 39]

وَيلٌ لِلمُطَفِّفينَ

Ole wao hao wapunjao!

الَّذينَ إِذَا اكتالوا عَلَى النّاسِ يَستَوفونَ

Ambao wanapo jipimia kwa watu hudai watimiziwe.

وَإِذا كالوهُم أَو وَزَنوهُم يُخسِرونَ

Na wao wanapowapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza.

أَلا يَظُنُّ أُولٰئِكَ أَنَّهُم مَبعوثونَ

Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa

لِيَومٍ عَظيمٍ

Katika Siku iliyo kuu,

يَومَ يَقومُ النّاسُ لِرَبِّ العالَمينَ

Siku watapo msimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote? [Al-Mutaffifin: 1-6]

Akawa Rasul (saw) anawasomea:

كَلّا ۖ بَل لا تُكرِمونَ اليَتيمَ

Sivyo hivyo! Bali nyinyi hamuwakirimu mayatima,

وَلا تَحاضّونَ عَلىٰ طَعامِ المِسكينِ

Wala hamhimizani kulisha masikini;

وَتَأكُلونَ التُّراثَ أَكلًا لَمًّا

Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa,

وَتُحِبّونَ المالَ حُبًّا جَمًّا

Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.
[Al-Fajr: 17-20]

**Itaendelea katika UQAB Toleo 16…In Shaa Allah.**



Email: info@uqab.or.ke

# SWALI/JAWABU: Ni Kipi Kilicho Nyuma ya Oparesheni ya Uturuki "Olive Branch" Kaskazini Mwa Syria?

**Swali**

Imegunduliwa kwamba harakati za Erdogan nchini Syria zimetulia kwa kiasi fulani baada ya oparesheni ya kuhami Furaat na kutelekeza kwa Erdogan mji wa Aleppo, na kuiruhusu serikali kuchukua udhibiti juu ya Aleppo, lakini akaregelea tena oparesheni hiyo kwa jina la 'Olive Branch' ikielekea eneo la Afrin tangu Jumamosi, 20/01/2018, kupitia mashambulizi ya anga ya silaha na makombora. Kwa mujibu wa taarifa iliyo tolewa na mkuu wa majeshi ya Kituruki mnamo Jumapili 21/01/2018: oparesheni ya Olive Branch, iliyoanza mnamo Jumamosi kwa mujibu wa mpango wake uliochorwa, na operesheni ya ardhini ikaanza mnamo Jumapili asubuhi. (Chanzo: Turk Press, 21/01/2018) na ambayo inaendelea, sasa ni kipi kilicho nyuma ya oparesheni hii ya "Olive Branch"? Allah akulipe kheri.

**Jibu**

1- Kabla ya kuanza kuchambua yaliyotokea, ni lazima tutulizie makini jambo moja muhimu mno linalounda msingi wa sera ya sasa ya Uturuki, litakalo angazia juu ya harakati za Erdogan na matendo na taarifa zake, kwa kuwa Erdogan wa Uturuki ni kibaraka waziwazi wa Amerika, anafanya hivyo kwa badali ya usaidizi wa Amerika ili kubakia mamlakani kama ilivyomleta mamlakani. Dalili ya hili ni yale yaliyotajwa na gazeti linalounga mkono serikali ya Uturuki la As-Sabah mnamo 18/4/2017: "Jana usiku Raisi wa Amerika alimpigia simu Raisi wa Uturuki Erdogan kumpongeza kwa matokeo ya kura ya maamuzi ya Aprili 16 juu ya marekebisho ya katiba na nidhamu ya uraisi".

Erdogan alimtajia kwamba "alianzisha kampeni nzuri kwa ajili yake na kwamba aliisimamia yeye mwenyewe". Alimwambia Erdogan: "Natilia maanani urafiki wetu na kuna vitu muhimu sana ambavyo tutafanya pamoja". Hivyo basi sera ya Erdogan nchini Syria kwa kweli ilikuwa ikisaidia mipango ya Amerika ya kumakinisha serikali ya Syria na kushinikiza makundi ya wapiganaji kujiondoa kutoka maeneo muhimu ya serikali hiyo. Mfano wa hili ni agizo la hivi karibuni la kuisalimisha Aleppo, na kuipa uwezo serikali hiyo, alibuni kadhia na kuyaondoa makundi ya wapiganaji yasipigane ndani ya maeneo yao ili yasiizuie serikali hiyo kuingia ndani ya maeneo hayo kwa kisingizio cha vita vya kuihami Furaat. Katika wakati ambapo serikali hiyo ilikwenda Aleppo na kuangazia mashambulizi yake huko, ikijua kuwa vita vya kuihami Furaat tayari vilikuwa vishapata baraka za Amerika, Uturuki iliingia eneo la Jarabulus mnamo 2016 kwa ushajiisho kutoka kwa Amerika wakati aliyekuwa Makamu wa Raisi wa Amerika Joseph Biden alipokuja jijini Ankara na kutangaza huko uungaji mkono wake wazi kwa kuingia jeshi la Uturuki mnamo 24/8/2016 na kuyataka majeshi hayo ya Uturuki ya vitengo vya ulinzi kujiondoa kutoka kwa majeshi ya Kituruki chini ya jina la ngao ya Furaat. Tumetaja katika Jibu la Swali mnamo 25/9/2016 kwamba: "Ili kuifanya mipango ya Amerika ifanye kazi, inayo angazia Aleppo, vikosi vya Uturuki ni sharti viekewe vizingiti vipya, na hapa Amerika imetumia mashoka mawili kuregesha uvamizi wa Aleppo: Kwanza: kuingiza jeshi la Uturuki kaskazini mwa Syria, kuanzia eneo la Jarabulus huku wakati huo huo Uturuki ikitangaza oparesheni "Kuhami Furaat" na kutoa wito kwa waasi wanaounga mkono Uturuki kutoka kusini mwa Aleppo kupigana na kundi la ISIS, yaani, kudhoofisha maeneo halisi ya mapambano mjini Aleppo! Na kuunda maeneo mapya ya mapigano na kuyasukuma makundi mengi zaidi ya upinzani kutokana na kupigana mjini Aleppo! nk". Hivi ndivyo namna Erdogan alivyo yaondoa makundi yaliyo na utiifu kwake kwenda kupigana katika maeneo ya Al-Bab na kuiacha Aleppo kuwa karibia huru kutokana na upinzani wowote, isipokuwa kwa waumini wachache waliosimama kidete. Huku haya yakijiri makundi mengi yaliitikia wito wa Erdogan wa kuihami Furaat na anarudia khiyana hii kwa mara nyengine tena.

2- Harakati hizi bado zingalipo zinazoiwezesha serikali ya Syria kuchukua udhibiti wa sehemu muhimu mjini Idlib na kuyaondoa makundi tiifu ya wapiganaji kwa maagizo ya Uturuki kuangazia juu ya Afrin na kusahau ardhi yao asili ya Idlib; ambayo serikali ya kihalifu inaisongelea kwa ushirikiano na Amerika, lakini chini ya kisingizio cha mizozo kati ya Uturuki na Amerika kuzuia matayarisho ya wanajeshi wapya wanao nasibishwa na Amerika! Tambua kwamba Amerika inasongea kutokea Uturuki kuelekea Syria na kuyahami kisilaha makundi yake vibaraka, ikiwemo vitengo vya ulinzi vya Wakurdi, ambao ndio idadi kubwa katika majeshi ya Kidemokrasia ya Syria yanayo nasibishwa na Amerika, ambapo Erdogan alifungua kambi ya Incirlik … Hivyo basi Erdogan anairudia hali ya Kuhami Furaat kurahisisha kuingia kwa serikali hiyo mjini Idlib. Oparesheni ya Olive Branch ilipangwa kurahisisha kuingia kwa serikali hiyo mjini Idlib.

Serikali ya Syria huku ikisonga kuelekea Idlib na kuuzingira uwanja wa ndege wa Abu al-Duhur, Erdogan ameyasukuma mapigano kuelekea Afrin!

Takriban makundi ya upinzani elfu 25 yanashiriki katika oparesheni hii kama ilivyo thibitishwa na kamanda wa kijeshi katika kikosi cha Sham, Yasser Abdul Rahim, kwamba

*Endelea Uk..14*

takriban wanajeshi waliojihami elfu 25 kutoka Jeshi Huru la Syria wanashiriki katika oparesheni ya kijeshi ya Uturuki mjini Afrin (Chanzo: Russia Today, 23/1/2018), yanayo julikana na Amerika pamoja na kuyapasisha kwake. Waziri wa Kigeni wa Uturuki Mevlüt Çavuşoğlu alisema kuwa alijadiliana na Waziri wa Ulinzi wa Amerika James Mattis juu ya mgogoro wa Syria na kadhia ya vitengo vya usalama mipakani mnamo Jumatatu jioni (15/1/2018) nchini Canada. Alisema kuwa pia alikutana na Waziri wa Kigeni wa Amerika Tillerson mnamo Jumanne jioni (16/1/2018) baada ya mkutano wa Mawaziri wa Kigeni juu ya usalama na uthabiti kwa kisiwa cha Korea jijini Vancouver, Canada. Çavuşoğlu alisema kuwa Mattis alisema:

"Tumeulizwa kutoziamini habari zinazo chapishwa kuhusu (kuundwa kwa jeshi jipya kaskazini mwa Syria)," akiongeza kuwa alikuwa "anaifuatilia kadhia hii yeye mwenyewe na atadumisha mawasiliano yake nasi." (Chanzo: Anadolu news agency 17/1/2018)

3- Hili linathibitisha taarifa za Amerika katika muda wa siku mbili zilizopita. Yanathibitisha kuwa Olive Branch, kadhia ya Afrin na harakati za jeshi la Uturuki na Jeshi Huru la Syria yote ni kwa kupasishwa kikamilifu na Amerika na Urusi, iliyo ingia Syria kwa ushirikiano na Amerika, hizi hapa ni baadhi ya taarifa hizo:

- Kampeni ya kijeshi ya Uturuki mjini Afrin ilianza jana Ijumaa, kwa hatua za kwanza za mashambulizi ya mabomu kwa baadhi ya maeneo ya Afrin kwa kasi kuu tangu Alhamisi/ Ijumaa usiku, kwa kuanza kwa kujiondoa kwa polisi wa kijeshi wa Urusi kutoka Afrin na vitongoji vyake. Nurettin Canikli aliikadiria kama "mwanzo wa mashambulizi ya ardhini," kwa mujibu wa runinga ya Al Jazeera … Al-Araby Al-Jadeed iligundua kutoka kwa chanzo cha Kituruki kwamba: "Ofa nyengine ilifanywa, kwa ajili ya kuudhibiti mji kwa badali ya makubaliano ya pamoja baina ya Ankara na Moscow katika namna ya usimamizi wao. Serikali ya Kituruki inahakikisha kwa kiwango kikubwa uundaji upya sawia na Kuhami Furaat, na kupitia kwa kushinikiza upinzani nchini Syria kuhudhuria kongamano la Sochi, huku Warusi wakisisitiza juu ya kuukabidhi mji baada ya kuudhibiti kwao na pia kuiruhusu serikali kufanya maendeleo zaidi katika mkoa wa Idlib.

Huku haya yakijiri, Waziri wa Ulinzi wa Uturuki Nurettin Canikli katika mahojiani ya runinga jana alithibitisha, "Tunajua kwamba Urusi inaisaidia serikali pakubwa" … Ama kuhusu matarajio ya Uturuki ya operesheni hii, chanzo cha Kituruki kiliiambia Al-Araby Al-Jadeed "Oparesheni hii inatarajiwa kuendelea kwa kiwango kisicho zidi miezi mitano hadi sita … Chanzo hicho kilitaja "mikondo hii ya kidiplomasia haikuathiri Washington." (Al-Araby Al-Jadeed, 20/01/2018)

"Mnamo 20 Januari, Uturuki aliamua kupeleka majeshi yake karibu na Afrin kaskazini magharibi mwa Syria … Moscow ina wasiwasi kuhusu habari hii," Wizara ya Kigeni ya Urusi ilisema katika taarifa, ikitaja kuwa ilikuwa "ikifuatilia kwa karibu maendeleo ya hali hii." "Urusi ingali imejitolea katika msimamo wake kuhusiana na kutafuta suluhisho ya mzozo nchini Syria, kwa msingi wa kuhifadhi hadhi ya eneo la nchi hii na heshima kwa ubwana wake," wizara ilisema). (Chanzo: Rudaw, 20/01/2018)

Amerika inataka operesheni ya kijeshi ya Uturuki kubakia kufungika kiwakati na kieneo, na kushauri "kujizuia kibinafsi" na kuhakikisha kuwa operesheni nyenginezo za kijeshi zinafungika kieneo na kiwakati, ili kupunguza uharibifu kwa maisha ya raia." Msemaji wa Wizara ya Kigeni ya Amerika Heather Nauert alisema, "Tunaisihi Uturuki kujizuia na kuhakikisha kuwa oparesheni zake za kijeshi zinabakia kufungika kieneo na kiwakati na zenye kuaminika kuepuka majeruhi ya raia." Waziri wa Ulinzi wa Amerika Jim Mattis alisema mnamo Jumapili kwamba Uturuki iliiarifu Amerika kabla ya hatua hiyo, akitaja kuwa Washington inawasiliana na Ankara kuhusu maendeleo ya hali hiyo. Alisema kuwa Waziri wa Kigeni Sergey Lavrov na mwenzake wa Amerika, Rex Tillerson, wamejadiliana juu ya "hatua ili kuhakikisha kuhifadhi uthabiti kaskazini mwa nchi". Waziri huyo wa Kigeni wa Uturuki alijadili operesheni ya kijeshi pamoja na mwenzake wa Amerika, lakini bado hakufichua yaliyotokea baina pande mbili hizo. (Chanzo: Shirika la BBC Arabic, 22/01/2018)

Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson alisema nchi yake inatarajia kufanya kazi na Uturuki kuasisi eneo salama kaskazini magharibi mwa Syria ili kufikia matakwa ya kiusalama ya Ankara… Kinara wa kituo kikuu cha utoaji amri za kijeshi cha Amerika, Jenerali Joseph Votel, alithibitisha kuwa Uturuki iliiarifu nchi yake kwa mukhtasari juu ya oparesheni zake za kijeshi mjini Afrin, akitaja kuwa mji huo hauko ndani ya mipaka ya eneo la oparesheni za kijeshi za Amerika.

Wizara ya Ulinzi ya Amerika inatoa wito wa "kutopalilia mzozo", ikitaja kuwa inafahamu wasiwasi wa kiusalama wa Uturuki eneo hilo. (Chanzo: Russia Today, 23/01/2018)

- Kituo Kikuu cha Utoaji Amri za Kijeshi cha Amerika kilisema Uturuki iliwaarifu kwa mukhtasari juu ya operesheni ya kijeshi katika mji wa Syria, Afrin, kikisisitiza wakati huo huo kuwa mji huo haumo ndani ya mipaka ya eneo la operesheni za kijeshi. Jenerali Joseph Votel, Kamanda wa Kituo Kikuu cha Utoaji Amri za Kijeshi cha Amerika, katika taarifa kwa vyombo vya habari mnamo Jumapili alisema kuwa nchi yake haitilii makini maalumu kwa eneo la oparesheni za Kituruki. (Chanzo: Quds Press, 21/01/2018)

- Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson alisema nchi yake inatarajia kufanya kazi na Uturuki kuasisi eneo salama kaskazini magharibi mwa Syria ili kufikia matakwa ya

*Endelea Uk..15*

kiusalama ya Uturuki; hii ilikuwa siku ya tatu ya operesheni Olive Branch iliyo anzishwa na majeshi ya Uturuki na Jeshi Huru la Syria. Eneo la mji wa Syria wa Afrin, Waziri wa Kigeni wa Amerika, “Wacha tuone ikiwa twaweza kufanya kazi na nyinyi ili kuunda aina ya eneo la usalama ambalo huenda mukahitaji… kwa hivyo tuko katika majadiliano na Waturuki na baadhi ya majeshi yaliyoko uwanjani pamoja na vipi tunaweza kutuliza hali hii na kutatua wasiwasi wa Uturuki kwa usalama wao.” (Chanzo: Turk Press, 23/01/2018)

- Na taarifa za Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson juu ya tangazo la nia ya nchi yake ya kuunda jeshi la wapiganaji elfu 30, ambao kazi yao ni “kulinda mpaka,” iliyo ikasirisha Ankara na kumfanya Tillerson kutoa maoni kwa maripota waliokuwamo ndani ya ndege ya serikali ya Amerika, “Nchi hii haina nia ya kubuni jeshi lolote la mipakani nchini Syria”.

Akiongeza kuwa kwa mujibu wa Anatolia, nchi yake inatoa ufafanuzi kwa ripoti za mashirika ya habari ya Uturuki za kuhusu nia ya Amerika kubuni jeshi la usalama mipakani nchini Syria, kwa hili, Nauert alisema, “Wapigeni vita kundi la ISIS, na hiyo ndio sababu halisi ya kuweko kwetu huko, na hiyo ni moja kati ya vitu ambavyo Waziri na wengineo katika Wizara ya Kigeni wameangazia kwa maafisa wa Kituruki.” (Chanzo: Orient, 19/01/2018)

- Jumanne iliyopita, msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Amerika Eric Bahon alisema nchi yake imefahamu wasiwasi wa Uturuki kuhusu jeshi la usalama mipakani inayopanga kuliunda nchini Syria, akitaja kadhia hii kwa maafisa wa Kituruki.

Bahon alitaja kuwa nchi yake iko katika mawasiliano ya karibu ya kila mara na Uturuki; mshirika wake katika NATO. Bahon alitumia maneno “jeshi tarajiwa la usalama mipakani” katika jibu lake … leo, Alhamisi, Waziri wa Kigeni wa Amerika Rex Tillerson alikuja kutangaza kwamba Amerika haikuwa na mipango ya kubuni jeshi lolote la mipakani nchini Syria, akitoa maoni juu ya ripoti za habari za kadhia hii. Aliongeza katika taarifa kwa vyombo vya habari: “Kadhia hii inahisiwa na kufafanuliwa kwa njia ya kimakosa, na baadhi ya watu wamezungumza kwa njia ya kimakosa, hatuundi jeshi lolote mipakani”. (Chanzo: Yenisafak Arabic, 17/01/2018)

Ni wazi kutokana na taarifa zilizopita kuwa Olive Branch ni tawi linalo bebwa na Uturuki kwa ushirikiano na Amerika na Urusi … na kwamba taarifa za Amerika mwanzoni mwa kubuniwa wanajeshi wa mipaka elfu 30 zilikuwa ni kuhalalisha tu operesheni ya Afrin, Amerika kisha ikabadilisha taarifa hiyo kwa namna ya kukataa wazi baada ya lengo lake kupatikana!

4- Hivyo basi, hatua za Uturuki nchini Syria ni za kutumikia miradi ya Amerika kwa kupanda nidhamu ya kisekula nchini Syria. Taarifa hizo za kelele kutoka kwa Erdogan ni kwa lengo tu la kuhadaa wajinga miongoni mwa watu kwa maneno makali na taarifa tasa zisokuwa na vitendo, kama wakati aliposema, hatutaruhusu Hama nyengine; lakini serikali hiyo ikatekeleza katika kila jiji na mji zaidi ya yaliyo fanyika Hama … pamoja na harakati bandia zisizo zalisha vitendo vya kiikhlasi. Aliwahadaa watu kwa taarifa za kupotosha zilizo wafanya wapumbavu wajinga miongoni mwa watu kama alivyosema kuhusu uamuzi wa Trump wa kuitambua Al-Quds (Jerusalem) kuwa mji mkuu wa umbile la Kiyahudi. Erdogan alitishia kukata mahusiano yake na umbile hilo la Kiyahudi endapo Jerusalem itatambuliwa kama mji mkuu wa umbile hili. Lakini hakukata mahusiano yake na Amerika iliyochukua uamuzi huu, bali badala yake inalisaidia umbile hili la Kiyahudi na kulipatia kila kitu kudumisha uhai wake. Pia alitoa wito wa suluhisho la Kiamerika la dola mbili, linalojumuisha kugurisha asilimia 80% ya Palestina kwa Mayahudi, na kutoa wito wa Jerusalem Mashariki kuwa mji mkuu wa Palestina, akiisalimisha Jerusalem Magharibi kwa Mayahudi hao. Hii ni kwa kuongezea yale aliyo yafanya na anayo endelea kuyafanya nchini Syria, na hata khiyana zake, zilizotilia nguvu uwepo wa maadui wa Kirusi na Kiamerika na serikali ya Syria, ima kupitia kuikabidhi Aleppo au kufungua kambi za Kiamerika ili kuingilia kati nchini Syria au kufungua anga ya Uturuki kwa ndege za Urusi au mikutano ya Astana, ambayo aliwashinikiza viongozi wa makundi ya kisilaha kukubali maamuzi yao na kuleta utulivu katika viwanja vya kivita na kupoza na kujiondoa kutoka maeneo na kuyasalimisha kwa serikali na kisha kuizingira Idlib na maeneo mengine zaidi. Hatimaye ikaja sura hii ya “Olive Branch” ili kuirahisishia serikali kuingia Idlib!

Mwisho, tunayahutubia makundi yote kwa kusema musidanganyike na vitendo vya Erdogan, na musiisalimishe Idlib kwa serikali … na wala musisahau yale yaliotendeka kwao mjini Aleppo, lakini kumbukeni hadith iliyo simuliwa na Bukhari kutoka kwa Abu Hurayrah (ra) kutoka kwa Mtume (saw) aliyesema:

**«لَا يُلْدَغُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرٍ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ»**

“Muumini hang’atwi mara mbili ndani ya shimo moja”. Sembuse kung’atwa mara nyingi?

**(إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ)**

“Hakika huo ni ukumbusho kwa yeyote mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.” [Qaf: 37]

**7 Jumada I 1439 H**
**24/1/2018 M**


2
BEVRIJD
JANNAT PISPALUF
BEVRIJD
JANNAT PISPALUF




#SaveJanat










BASHAR
STEP
PROTESTMARCH
MOD BLODSUDGYDELSERNE I
SYRIEN